Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA ZA WAJUMBE WA KAMATI YA UCHAGUZI WA UONGOZI WA TAASISI

Uongozi wa Taasisi ya SETTA unatangaza rasmi kuanza kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Uongozi wa Taasisi utakaofanyika tarehe **28 Novemba, 2026**.

Ili kuhakikisha zoezi hili linaendeshwa kwa misingi ya Haki, Uwazi, Uadilifu, na Ufanisi wa hali ya juu, Taasisi inaakaribisha maombi kutoka kwa Alumni wenye sifa na nia ya kujitolea kuwa wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi.

Nafasi zinazotangazwa ni **tatu (3)**. Kwa mujibu wa kanuni za uwianisho na ulinganifu wa jinsia wa Taasisi ya SETTA, **angalau nafasi moja (1) kati ya hizo tatu lazima ijazwe na mwanamke**.

MAJUKUMU MAKUU YA KAMATI YA UCHAGUZI

1. Kuandaa, kuratibu, na kusimamia mchakato mzima wa uchaguzi kuanzia hatua ya utoaji wa fomu hadi kutangaza matokeo rasmi.
2. Kuhakikisha kanuni, sheria ndogo, na mwongozo wa uchaguzi wa SETTA unafuatwa kikamilifu.
3. Kupokea, kuchuja, na kuhakiki sifa za wagombea wote wa nafasi mbalimbali za uongozi.
4. Kusimamia zoezi la upigaji na uhesabuji kura siku ya uchaguzi (**28 Novemba, 2026**).
5. Kutatua malalamiko au mizozo yoyote itakayojitokeza wakati wa mchakato wa uchaguzi kwa haki na bila upendeleo.

SIFA MUHIMU ZA MUOMBAJI

Muombaji wa nafasi hii ya kujitolea anapaswa kuwa na sifa na vigezo vifuatavyo:

1. **Uadilifu na Maadili Mema:** Awe na maadili, mwaminifu, na asiyewahi kuhusika na vitendo vya ukiukaji wa maadili au nidhamu.
2. **Kutokuwa na Mgongano wa Maslahi:** Muombaji asipange wala asiwe na nia ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi katika uchaguzi mkuu wa taasisi.
3. **Msimamo Huru na Usio na Upendeleo:** Uwezo wa kusimamia haki bila kuonyesha mahusiano au upendeleo kwa mgombea au kundi lolote.

SETTA
SOCIAL-ECONOMIC TIER OF TURKISH ALUMNI

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

4. **Ujuzi wa Uratibu na Usimamizi:** Uwezo wa kufanya kazi kwa ushirikiano katika timu, kusimamia migogoro, na kuratibu shughuli za uendeshaji kwa umakini.

5. **Uwezo wa Mawasiliano:** Uwezo mzuri wa kuwasiliana kwa ufasaha, kwa maandishi na maongezi.

6. **Utayari na Upatikanaji:** Uwezo wa kutenga muda wa kutosha kuanzia hatua za maandalizi ya uchaguzi hadi siku kuu ya uchaguzi (**28 Novemba, 2026**).

7. **Kigezo cha Jinsia:** Wanawake wanahimizwa kwa dhati kuomba ili kutimiza sharti la kikanuni la **mwanamke mmoja (1)** katika kamati ya watu 3.

ASILI YA UTEUZI (AINA YA KAZI)

Nafasi hizi ni za **kujitolea**. Wajumbe watakaoteuliwa watatumikia Taasisi kwa misingi ya uzalendo, kujenga uzoefu wa usimamizi wa michakato ya kidemokrasia, na kutoa mchango katika ujenzi wa uongozi bora wa taasisi ya SETTA.

TARATIBU ZA UTUMAJI WA MAOMBI

Waombaji wote wanaokidhi sifa wanatakiwa kuwasilisha nyaraka ifuatayo:

- **Barua ya Maombi** inayoeleza nia na utayari wa kujitolea kuwa sehemu ya Kamati ya Uchaguzi.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya Barua Pepe au kuwasilishwa physically ofisini kabla ya **Tarehe 15 Novemba, 2026, saa 11:00 Jioni**.

- **Anwani ya Barua Pepe:** info@settafoundation.or.tz
- **Kichwa cha Barua Pepe:** “Maombi ya Wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi 2026”.

ZINGATIA: *“Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda wa mwisho hayatapokelewa. Maombi yenye taarifa za kughushi yatasababisha muombaji kuondolewa sifa mara moja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu”.*

Imetolewa na:

SOCIAL ECONOMIC TIER OF TURKISH ALUMNI (SETTA) P. O. BOX 6166 DAR ES SALAAM – TANZANIA

Mwenyekiti,
Kamati ya Uchaguzi,
Taasisi ya SETTA.
Tarehe: 05 Novemba, 2026.